

TAARIFA YA UTEKELEZAJI MRADI WA MAJI CHALINZE AWAMU YA TATU

1.0 UTANGULIZI;

Mradi wa Maji Chalinze awamu ya tatu ni mojawapo ya miradi ya kimkakati uliosanifiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wananchi wa Halmashauri ya Chalinze, Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Pwani, Ngerengere na baadhi ya vijiji vya Mkoa wa Morogoro.

1.1 KUANZA KWA MRADI

Mradi ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 na DAWASA kupitia Mhandisi Mshauri wa Kampuni ya ujenzi ya Afcons (Afcons Construction Limited) kwa lengo mahususi la kuondoa tatizo la upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa maeneo tajwa.

1.2 UTEKELEZAJI WA MRADI

Utekelezaji wa mradi umehusisha kazi mbalimbali ikiwemo kazi ya upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Wami kwa lengo la kuongeza uwezo wa uzalishaji maji kutoka lita 500,000 za maji za sasa mpaka lita 900,000 ili kuweza kuhudumia wakazi wa Halmashauri ya Chalinze, Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga, baadhi ya vijiji vya mkoa wa Morogoro, Mkoa wa Pwani na eneo la Ngerengere.

Kazi nyingine iliyotekelezwa ni ujenzi wa matenki 19 ya kuhifadhi maji yenye ujazo wa lita 500,000 mpaka lita milioni 2 yanayojengwa kwenye maeneo ya Kimange, Rupungwi, Mandela, Hondogo, Kilemela, Miono, Msata, Kihangaiko, Mazizi, Saleni, Lugoba, Mindutulieni, Diozile, Msoga, Bwiligu, Mpera, Pingo, Manga na tenki la Majisafi Mtamboni.

Pia mradi umehusisha kazi ya ujenzi wa vioski (vizimba) 351 vya kuchotea maji ambavyo vimejengwa kwenye vijiji zaidi ya 69 na vimekamilika, baadhi ya hivyo ni kijiji cha Msingi, Mdaula, Msolwa, Visakazi, Kikaro, Buyuni, Mandamazingara na kijiji cha Mboga kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa huduma ya maji kwa urahisi kwa vijiji zaidi ya 69.

Utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji Chalinze awamu ya tatu unalenga kuhudumia zaidi ya wakazi 200,000 wa Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze na maeneo mengine tajwa.

Mbali na hapo mradi umejenga mtandao wa mabomba makubwa ya inchi 12 na 16 ya kusafirisha maji kwa umbali wa kilomita 24, pamoja na ujenzi wa mabomba ya kusambaza maji kwa umbali wa kilomita 1,268.

Mradi unatarajiwa kunufaisha wakazi wa Halmashauri ya Chalinze, sehemu ya kata zilizopo Tanga, Mkata, Morogoro na Bwawani mkoa wa Pwani. Pia kata ya Kiwangwa, Msata, Miono, Magomeni, Vigwaza, Tarawanda, Bwirigu, Ubena zomozu, Mbwewe, Lugoba, Fukayose, Mpera, Msoga kimange, Mandela, Gwata, Magigu, Mkata kwa sungu, Ngerengere na Kidugalo.

Kupitia utekelezaji huu, mradi utakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 22 za maji ambayo ni ziada ya mahitaji ya maji kwa Halmashauri ya Chalinze ya lita 7 – 9 kwa siku.

1.3 HALI YA UTEKELEZAJI WA MRADI KWA SASA

Mpaka sasa mradi umetokelezwa kwa asilimia 96 na kazi inaendelea ya kukamilisha sehemu iliyobaki kufikia asilimia 100.